GRADE 8 KLB TOP SCHOLAR KISWAHILI LESSON PLANS TERM 1

SCHOOL	LEVEL	LEARNING AREA	DATE	TIME	ROLL
	Grade 8	KISWAHILI			

WIKI: 1 NAMBARI YA SOMO: 1

MADA NDOGO: Kusikiliza na kuzungumza; Kusikiliza na kujibu

MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA: Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze;

a) Kueleza kuhusu picha aliyoitazama katika kitabu cha mwanafunzi.

b) Kusikiliza mahojiano kati ya mwalimu na mwanafunzi.

c) Kutaja vitendo ambavyo mhojiwa alifanya kuonyesha kuwa alisikiliza mahojiano.

d) Kukuza ubunifu wa usikilizaji.

MASWALI DADISI:

Je, unaposikiliza mtu akizungumza unafaa kufanya nini ili uupate ujumbe kiukamilifu?

NYENZO:

KLB; Top Scholar; Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Gredi ya 8, Uk. 1-2, Kapu maneno, Chati, Mabango, Kamusi, Majarida, Michoro na picha, Vifaa vya kidijitali

MPANGILIO WA MASOMO: Ndani ya darasa/wafanye kazi kwa vikundi, wakiwa wawili na wakiwa pekee yao.

MWONGOZO WA SOMO

WAKATI	MADA
DAKIKA 5	**MWANZO** Mwalimu atangulie kwa kuwakaribisha wanafunzi darasani. Mwalimu atangulie kwa kuuliza swali k.v. Je, unaposikiliza mtu akizungumza unafaa kufanya nini ili uupate ujumbe kiukamilifu?
DAKIKA 20	**UWASILISHAJI** **Hatua 1** Wakiwa wawili, wanafunzi amweleze mwenzake kuhusu picha aliyoitazama. **Hatua 2** Wanafunzi waweze kusikiliza mazungumzo kati ya mwalimu na mwanafunzi. **Hatua 3** Wanafunzi waweze kutaja vitendo ambavyo mhojiwa alifanya kuonyesha kuwa alisikiliza mahojiano.
DAKIKA 5	**KAZI YA ZIADA.** Wanafunzi kujadiliana na mzazi/mlezi kuhusu vipengele vya kuzingatia katika mahojiano. **HITIMISHO** Mwalimu asikilize baadhi ya wanafunzi wakisoma na kutambua vipengele vya kuzingatia katika usikilizaji wa mazungumzo

MAONI…….